

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MANYARA. HUDUMA ZA MAGONJWA YA MACHO ZITOLEWAZO



Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Manyara inatoa huduma kwa wateja wa ndani ya Mkoa wa Manyara na wateja wa nje ya Mkoa. Hata hivyo huduma zinazotolewa zinaendelea kuboresha zaidi kupitia Wizara ya Afya pamoja na wadau wa Afya hasa kwa kushirikiana na Shirika la Kilimanjaro Centre for Community Ophthalmology (KCCO) katika utekelezaji wake kwa kuhakikisha inatoa huduma ya matibabu ya macho kwa jamii ya watu wa Mkoa wa Manyara na Mikoa ya Jirani.

Baadhi ya huduma zinazotolewa katika kitengo cha Macho ni pamoja na ;

1. Uchunguzi na upimaji wa macho/Eye examination

- ❖ Uchunguzi huu unahusisha magonjwa ya Kioo cha mbele cha Jicho (kovu la Kioo cha Jicho, ukungu wa Kioo cha Jicho, Macho mekundu, Muwasho wa macho, ukavu wa macho.
- ❖ Uchunguzi wa athari zitokanazo na Ugonjwa wa Sukari na presha.
Magonjwa ya ndani ikiwemo sukari na presha yameathiri kwa kiasi kikubwa uono kwa wagonjwa wengi wa macho

2. Huduma ya Vipimo vya macho/Diagnostic services

Vipimo hivi husaidia kujua hali ya ugonjwa , kiwango cha athari pamoja na matibabu sahihi , vipimo vinahusisha upimaji wa yafuatayo;

- ❖ Presha ya macho (Glaucoma)
Tatizo hili husababishwa na kuongezeka presha ya jicho (intraocular pressure) kutokana na kukosekana uwiano wa mzunguko wa majimaji ndani ya jicho (aqueous fluid) kinachotoka kidogo kuliko kinachoingia.
- ❖ Upimaji wa lensi Kwa kutumia mawimbi ya sauti n.k



3. Huduma ya Upasuaji wa Macho/Surgical eye services

Huduma hizi zinatolewa hospitalini kwa utaratibu uliowekwa na zinatolewa kwa uharaka na kwa ufanisi zikihusisha;

- ❖ Upasuaji rekebishi/Usafishaji wa mtoto wa jicho(cataract) Kwa wazee na wenye tatizo la uoni wenye wingu/hafifu.
- ❖ Upasuaji wa uvimbe kwenye jicho
- ❖ Upasuaji wa vinyama kwenye jicho na huduma nyingine nyingi za upasuaji na ushauri.

4.Huduma za Miwani/Optomety Services

Hospitali inatoa huduma ya miwani kwa kuzingatia vipimo vilivyofanyika na kujiridhisha miwani gani itafaa kwa mgojwa.

Aina ya miwani zitolewazo ni pamoja na ;

❖ **Miwani za kusomea- reading glass**

Miwani ya kusoma ni aina ya miwani ya macho, ambayo hutoa glasi za myopia zinazotumiwa sana na watu wenye presbyopia, ambayo ni ya lens ya convex. Miwani ya kusoma hutumiwa kujaza macho ya watu wa makamo na wazee. Kama glasi za myopia, zina viwango vingi vya kiashiria vya kielektroniki vinavyohitajika na viwango vya tasnia ya kitaifa, na pia vina kanuni za kipekee za matumizi. Kwa hiyo, miwani kwa ajili ya kusoma lazima ziwe na glasi.

Miwani kutoona mbali (short sightedness)

Magonjwa haya ya macho Hayana umri maalumu na huitwa B. Myopia '. yanaweza kumpata mtu wa umri wowote. Ugonjwa huu unaweza kusabisha kichwa kuuma kwa muda mrefu . Matibabu yake ni pamoja na kuvaa miwani yenye kuongeza mbali.

❖ **Miwani za uoni wa karibu**

Magonjwa ya macho ya Kutoona karibu (long sightedness) , Tatizo hili mara nyingi huwatokea watu wenye umri wa miaka 40 na kuendelea.

❖ **Miwani za kupunguza mwanga**

Hospitalini inatoa miwani hizi ili kusaidia kwenye jua, mwanga, na wakati wa kuangalia Runinga/ television na kusaidia kupunguza mwanga wakati wa kutumia laptop

Hospitali inaendelea na Utoaji wa elimu ya Afya ya macho kupitia vipeperushi, huduma za kliniki Mkoba, Radio pamoja na televisheni ili kuweza kuwafikia wananchi wote ndani na nje ya Mkoa wa Manyara.